

Misimamo (Hatua) za tarehe Moja Julai

Ingilio

Serikali imechukua hatua (misimamo) za kuzuia kusambaa kwa janga la virusi ya corona. Heshimuni misimamo hiyo. Hivyo basi, tunaepuka kupata magonjwa hayo na kuambukiza watu wengine. Polisi inahusika nakuchunguza heshima ya misimamo hizo.

Misimamo za Msingi

- Ikiwa unauguwa, baki nyumbani kwako.
- Nawa mikono mara na mara kwa maji safi na sabuni.
- Heshimu umbali wa mita moja na nusu kwa kutengana na wengine.
- Inawezekana kuwa na mawasiliano na watu kumi na tano kwa wiki kwa kiwango cha juu. Ni heri zaidi mawasiliano haya yafanyike nje.
- Unapatikana kwenye mahali ya umma (nafasi ya kungojea gari, sokoni, dukani,...) ambapo ni kugumu kutengana karibuni mita moja na nusu ? Lazima uvae barakoa ao mask yako.
- Uwe kila mara na barakoa ao mask yako popote uendapo.

Kusafiri kwenye jiji lingine ao ugenini.

- Katika Ubeljiji :
 - Unaweza safiri ukiwa huru.
 - Unatumia uchukuzi wa pamoja (basi, lorry, tremu) ? Unazaidi ya myaka kumi na mbili ? Vaa barakoa ao mask ao kitambaa yenye kufunika vizuri kwa pamoja kinywa na pua.
- Ukiwa likizoni ugenini :
 - Unaweza kusafiri tu kwenye mojawapo wa nchi za umoja wa Ulaya (Union européenne), Uingereza ukiwemo (Royaume-Uni), pia Uswisi (Suisse) , Islande, Liechtenstein na Norway (Norvege).
 - Misimamo (hatua) hizi zinaweza kubadilika kadiri ya nchi. Misimamo hizo zinapatikana kwenye mtandao https://diplomatie.belgium.be/nl/Diensten/Op_reis_in_het_buitenland/reisadviezen.

Kazi

- Ikiwezekana, tumikia nyumbani kwako.
- Ni lazima kwenda ofisini ? Mwajiri n(mwenyeji kazi) analazimishwa kuheshimu hatua za kutengana kwa mita moja na nusu kwa wafanya kazi. Kama sivyo, ? Omba barakoa ao mask kwa mwajiri kwa kujikinga.
- Una ulizo ? Mwajiri wako atakujibu (atakupa maelezo).

Biashara

- Duka zote zimefunguliwa
- Duka za usiku zimefunguliwa hadi saa saba ya usiku.
- Soko ya adharani zimeruhusiwa.
- Unaweza kujielekeza kwa kinyozi ao kwa mtengeneza nywele
 - Kabla ya kujielekeza huko, mukubaliane mpango ya pamoja mteja na kinyozi.
 - Vaa barakoa ao mask yako.

Sekta ya Hoteli na Upishi

- Mahali pa kuuzisha vinywaji, mgahawa ama restorenti zimefunguliwa hadi saa saba ya usiku.
 - Ni heri zaidi kwa wateja kupatanisha chakula wala kinywaji mbele ya wakati.
 - Kwa kiwango cha juu, kundi lisitambuke hesabu ya watu kumi na tano.
 - Baki kwenye kiti chako ukiwa kando ya meza yako bila kutangatanga.

Mawasiliano za kijamii

- Kila mtu anaweza kuwa na mawasiliano za karibu na watu kumi na tano mbalimbali kila wiki.
 - Inaombwa kukutana nje ya nyumba.
 - Aiwezekani mukutane nje ya nyumba ? Ni lazima kuingiza hewa nyingi nyumbani : fungueni dirisha.
- Munapendelea kufanya shughuli kati ya kundi (kwa mfano kwenda kwenyi restorenti, ao kufanya matembezi, ao kuandaa mapokezi nyumbani) ? Mikusanyo kama hizo zinaruhusiwa bila kutambusha hesabu ya watu kumi na tano kwa kiwango cha juu.

Mazoezi.

- Munaweza fanya michezo katika kundi lisilo tambuka hesabu ya watu makumi tano kwa kiwango cha juu. Heshimuni umbali wa mita moja na nusu kwa kiwango cha chini.
- Munaweza fanya michezo ndani ya senta ya uzima ao ndani ya klabu ya michezo ao ndani ya visima ya kuogelea.
- Chumba cha kuogea maji yenye unyevunyevu (saunas) na nyumba ya ustawi (ama ya afya bora) (centres de bien – etre) vimefunguliwa kwa umma.

Burudani

- Tokea tarehe moja julai, nafasi zote za burudani zimefunguliwa kwa mfano maktaba, nafasi za kivutio, uwanja za michezo na kasino.
- Unajielekeza kwenye kituo rasmi (kwa mfano : karamu ya kijiji, mashindano ya michezo ao tukio la kitamaduni) ? Kunako mpaka wa nafasi kwa kiwango cha juu :
 - Tokea tarehe moja julai : Watu mia mbili ndani, watu mi aine nje.
 - Tokea tarehe moja agosti : Watu mi aine ndani, watu mia nane nje.
- Misimamo zinaweza badilika kufuatana na chama ao miungano.
- Kwa watoto, kambi zinaweza kuandaliwa.

Nini Hairuhusiwi mpaka sasa ?

- Chumba cha kusikilizia na kuchezea musiki ao vilabu vya usiku haviwezi kufungua bado.
- Tukio kubwa (kwa mfano tamasha ama sherehe kubwa) haviruhusiwi bado.

Dini

- Ibada za dini na madheehebu mbalimbali zinaruhusiwa.
 - Kiwango cha juu, mukiwemo watu mia mbili
 - Kukaribiana kimwili, kwa haizuru namna gani, kunakatazwa.

Mahali ya ulinzi ya watoto na shule

- Mahali ya ulinzi ya watoto zimefunguliwa. Les crèches sont ouvertes.
- Masomo yako ikujulishe kuusu mwaka wa masomo ufuatao. Votre école vous renseigne sur l'année scolaire prochaine.

Faraja

Misimamo ama hatua hizi ni za lazima kwa kuinga afya ya umma. Kila mmoja analazimishwa kuziheshimu . Asante kwa mchango wako. Kwa pamoja, wote tunagombanisha janga la virusi ya corona.